

HALMASHAURI YA JIJI ARUSHA



TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI NA.LGA/003/2017-2018/NC/07

YA

ZABUNI YA WAKALA WA UKUSANYAJI WA MADENI YA WADAIWA SUGU WA WA USHURU WA MABANGO NA HUDUMA

1. Halmashauri ya Jiji la Arusha inakusudia kutumia huduma za wakala wa kukusanya Madeni yake kwa wadaiwa mbalimbali
2. Halmashauri ya Jiji la Arusha inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao kwa zabuni ifuatayo

NAMBA YA ZABUNI	MAELEZO YA ZABUNI	ADA YA ZABUNI
LGA/003/2017-2018/NC/07	Wakala wa Ukusanyaji wa Madeni ya Halmashauri	50,000

3. Mzabuni atatatakiwa kukusanya Madeni kulingana na orodha ya madeni itakayotolewa na Halmashauri ya Jiji na kwa viwango vilivyowekwa na Jiji
4. Wakala anahitajika kuomba zabuni kwa kutaja kamisheni ikiwa asilimia atakachorejeshewa na Halmashauri ya Jiji kutoka katika makusanyo/Mapato aliowasilisha kwa kila mwezi
5. Zabuni zitashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindani wa kitaifa [National Competitive Bidding] ulioanishwa kwenye Kanu/78ni za Manunuzi-[The Public Procurement - goods, works, non-consultant services and disposal of Public Assets by Tender]. Regulations, 2013 na The Local Government Authorities Tender Boards [establishment and proceedings] regulations, 2014 na iko wazi kwa waombaji wote wa hapa nchini.
6. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili kupitia makabrasha ya zabuni katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Jiji la Arusha, barabara ya Boma S.L.P. 3013, Arusha, kila siku kuanzia saa 2.30 asubuhi hadi saa 9:00 Alasiri, siku za Jumatatu hadi Ijumaa [kuondoa siku za sikukuu zinazotambulika kitaifa]

7. Nyaraka za aina zote za Zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada stahili ya zabuni husika kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lililopo namba mbili hapo juu. Malipo ya maombi ya zabuni yanaweza kufanyika kupitia akaunti ya Halmashauri ya Jiji la Arusha iliyoko katika Benki ya NMB, tawi la Clock Tower, akaunti ya Jumla [General Fund Account] ya Jiji la Arusha namba 40801200336 na kuwasilisha nakala halisi ya hati ya malipo ya Banki [Bank Pay-in Slip, original copy] na kupata stakabadhi ya Halmashauri kwa zabuni iliyoombwa. Malipo yaliyotolewa kama ada ya maombi ya zabuni hayatarejeshwa.
8. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja Maelezo ya zabuni, namba ya zabuni na Zabuni hizo zipelekwe katika sanduku la zabuni lililoko katika ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji Kwa kupitia Anuani ifuatayo;

KATIBU WA BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA JIJ
S.L.P 3013
ARUSHA.

9. Muda wa mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni **tarehe 23 .6. 2107 saa 4:00 asubuhi**. Maombi yote yatafunguliwa muda mfupi baadaye na kwamba waombaji wote au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo.
10. Halmashauri ya Jiji la Arusha hailazimiki kukubali/ kutokukubali kutoa zabuni kwa mwombaji zabuni yeyote kutokana na kigezo cha malipo makubwa/malipo kidogo ya zabuni.
11. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha.
12. Mwombaji aliyewahi kushitakiwa kuhusiana na ukiukwaji wa kazi za ukusanyaji wa mapato, hatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi yeyote ya zabuni iliyotangazwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha. Vile vile mawakala watakaothibitika kuwa na tuhuma za utendaji usiozingatia sheria kutoka taasisi nyingine za Serekali hawatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi zinazotangazwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha.
13. Maelekezo yote yaliyotolewa katika tangazo hili pamoja na yale yaliyoko katika nyaraka za maombi ya zabuni ni sehemu ya masharti kwa mwombaji wa zabuni.

MKURUGENZI WA JIJ
HALMASHAURI YA JIJ LA ARUSHA
SLP 3013 Arusha, Tell, No. 2508073/2503494
[E-mail](mailto:cd@arushacc.go.tz)[cd@arushacc.go.tz](http://www.arushacc.go.tz) Web site: www.arushacc.go.tz